

TANGAZO

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwajulisha watu wote wanaotaka kufanya Mtihani wa Kidato cha Sita (**ACSEE**) mwezi **Mei, 2021** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Kipindi cha usajili kwa watahiniwa wa Kujitegemea kimeanza tarehe **1 Julai** hadi **30 Septemba, 2020** kwa ada ya Shilingi **50,000/=**. Aidha, watakaojisajili kwa kuchelewa yaani tarehe **01/10/2020** hadi tarehe **30/10/2020** watalipa Shilingi **65,000/=** ikiwa ni ada ya kawaida pamoja na faini.
2. Kabla ya kujisajili kwenye mtandao, waombaji wanapaswa kwenda kwenye Vituo vya Mitihani kuchukua namba rejea (**reference number**) zinazotolewa **bure** na kufanya malipo ya ada kupitia Posta au Benki kwa kutumia 'Control Number'.
3. Ufafanuzi kuhusu utaratibu wa hatua za kufuata katika kutengeneza 'Control Number' na kujisajili, umetolewa katika tovuti www.necta.go.tz. Aidha, kwa Watahiniwa ambao **hawataweza** kutumia mfumo huo, wafike ofisi za Posta kwa msaada zaidi.
4. Waombaji wote **wanasisitizwa** kuhakikisha wanajisajili mapema kwani mfumo wa usajili utafungwa baada ya kipindi cha usajili kumalizika.

Imetolewa na:

KATIBU MTENDAJI